J W McGarvey Kuhusu Vikombe Vingi

(J W McGarvey On Individual Cup)

Ifuatayo ni nukuu kutoka kwa J W McGarvey, hayati rais wa Chuo cha Biblia, Lexington, Kentucky, na anakubali kuwa yeye ni mmoja wa wale wanafunzi wakuu katika enzi zake.

“Karibia miaka miwili iliyopita, nadhani nilichapisha kipeperushi chenye kichwa cha habari ‘Vijidudu’, ambayo nilidhihaki kwa njia ambayo nilidhani inafaa, kutetea matumizi ya vikombe vingi katika Meza ya Bwana. Maelezo ya ‘usafi’, kama Ndugu Keeler anavyoiweka katika mtindo, inathibitika kuwa ni majigambo kwa ukweli kwamba hata kama matumizi ya vikombe imezoeleka kuwa ni ya dunia nzima na imekuwa ikitumika karibia miaka elfu mbili, hakuna tukio hata moja iliyotolewa ya mtu kupata maambukizi ya ugonjwa kutoka katika kikombe. Na kama kungekuwa na matukio machache, au maelfu wachache miongoni mwa mamilioni mengi, hiyo inalinganishwa na uchunguzi wa hali ya juu kwa agizo lililotolewa na Bwana Yesu Kristo?

Je tunapaswa kujaribu kubadilisha au kuboreshaa agizo kama hilo kwa kuhofia mmoja wetu anaweza kuthibitisha kuwa miongoni mwa mamilioni wanaoweza kuathirika? ‘Vipengele vya usafi’ kama kila mmoja anavyofahamu imewekwa kwa umakini unaofaa dhidi ya agizo la ubatizo maana ilianzishwa na Kristo, na imekuwa kwenye msitari kama kithibitisho cha wale wanao iboresha aagizo hili. Uhaba wa kutofikiri katika matukio yote mawili inaleta hofu kwamba hitaji la imani, na sio hakika kuogopa ugonjwa na kifo, ikiwa chini yake. Ikiwa kuna hatari ya kumeza mdudu kwa kukinywea kikombe hicho hicho, vipi kuhusu kubatizwa katika maji yaleyale? Je tunapaswa kutoa maji katika sehemu ya kubatizia, tupasafishe, na kuweka kemikali kila baada yaa ubatizo? Kama sivyo, je mara zote tunapaswa kutafuta maji yanayo tiririka, ambamo mbwa aliyekufa anaweza kuonekana karibu nasi? Au tunapaswa kuacha ubatizo jumla kwa sababu ya kuwaweka watu wetu wasiathirike na wadudu wasiooenekana wanaohama kutoka kwa majirani zetu?

Watu wengine ni wazuri kwa ulimwengu huu. Wanapaswa kubeba chupa inayonuka kwa siku zao zote na kumwomba Bwana awachukue haraka iwezekanavyo waende katika nchi yenye afya. Ni wazo langu kwamba Bwana alipoanzisha meza ya Bwana alifahamu zaidi kuhusu vijidudu kama ilivyo kwa wauguzi wa leo.”

Ignatius kuhusu kikombe

Matumizi ya kikombe kimoja, kama ilivyoanzishwa na Bwana, inarudi nyuma katika historia karibia siku za Mitume, kama Ignatius alivyoandika baada ya sehemu ya kwanza ya karne ya kwanza.

“Mwana kuna mwili mmoja wa Bwana Yesu Kristo, na damu yake imwagikayo kwa ajili yetu ni mojaa. Mkate mmoja unamegwwa kwa ajili ya wote, na kikombe kimoja hugawanywa miongoni mwao wote.”

“Anti-Nicene Father, Tol. 1, Uk. 81).